ShuleyaSekondariKiwira,
S. L. P 776,
TUKUYU.

Simu: 0758451535/0765889090

Tarehe …………………………...

Jina la Mwanafunzi……………………………………

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIWIRA MWAKA 2021**

**1.0 Utangulizi:**

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo 2021. Shule ya sekondari Kiwira ipo umbali wa kilomita $1^{3}/_{4}$ mashariki mwa mji mdogo wa Kiwira katika halmashauriya wilaya ya Rungwe. Muhula wa kuanza masomo unaanza **11/01/2021,** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021.

**2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia ambayo mwanafunzi anatakiwa kuja nayo:**

2.1 **Sare za shule**:

a) Sare ya shule hii ni suruali mbili rangi ya bluu na kijani, kwa wavula na inatakiwa iwe na marinda mawili na turnup chini na kwa wasichana ni sket imbili ndefu rangi ya bluu na kijani yenye marinda ya kawaida yasiyopungua 10.
b) Rangi ya Hijab ni nyeupe isiyo na maua
c) Viatu vyeusi vya kamba vyenye kisigino kifupi kwa wavulana na wasichana.
d) Soksi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
e) Wavulana wawe na mkanda mweusi usio na chata yoyote.
f) Sweta mbili zenye shingo ya ”V” rangi ya bluu na nyingine rangi ya kijani.

2.2 **Vifaa vya taaluma:**

- Daftari counter book Quire 2 au 3 ziwe 10
- Daftari za mazoezi [msomi] ziwe 10
- Rula ndefu nyeupe [30cm]
- Mkebe wenye vifaa vyote [oxford]

2.3 **Chakula**

Chakula cha mchana kwa mwanafunzi wa kutwa ni lazima na kinachangiwa na mzazi/mlezi kutoka kwenye makubaliano ya vikao vya wazazi/mlezi.

2.4 **Afya**

Mtoto awe na Bima ya Afya (NHIF) au Bima ya jamii (CHF)

**2.5 Vifaa vya usafi:**

- Fagio la chelewa kubwa
- Ndoo ndogo ya lita 10
- Kwanja la kufyekea 1

**3.0 Sheria na kanuni Muhimu za Shule hii:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na25 ya mwaka1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu sayansi na teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayoa mbayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine, jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni [preparation].
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
h) Kutunza mali za umma.

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:**

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi maliya umma.
g) Kudharau Bendera yaTaifa.
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:**

a) "Medical Examination Form" ambayo itajazwa na Mganga Mkuuwa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi/ mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.
e) Namba ya simu ya mzazi/mlezi.

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII,

JOEL MSAFIRI
*MKUU WA SHULE*

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**
**SHULE YA SEKODNARI KIWIRA**

## A. FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOZA YA JINAI

**MKUU WA SHULE,**
**SHULE YA SEKONDARI KIWIRA,**
**S. L. P 776,**
**TUKUYU.**

**[MAELEZO YA MWANAFUNZI]**

Mimi ………………………………………………………………..

Mahali ninapoishi kijiji cha ……………………………………...

Nimemaliza shule ya msingi ……………………………………..

Katika mika saba ya elmu ya msingi nimewahi/sijawahi kufanya mgomo/fujo/kosa la jinai

Nakiri na kukuali kutoshiriki mgomo/fujo/kosa la jinai kwa muda wote nitakao kuwa shuleni.

Sahihi ya mwanafunzi ………………………………..

## B. UKIRI WA MZAZI NA KUKUBALI SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZOTE ZA SHULE

Mimi …………………………………………………..

Ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi …………………………………… Nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu zote za shule na maelezo mengine yatakayotolewa na shule, pamoja na kumhimiza motto kuja shule kila siku.

Sahihi ya mzazi/mlezi ………………………………..

KARIBU SANA KIWIRA SEKONDARI

………………………
MKUU WA SHULE

**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**

KIWIRA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 776,
TUKUYU.

Date: ………………

To Medical Officer,
…………………………..
…………………………..
........................................

PART A

Mr./Miss …………………………………………

Please, examine the above named pupil as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories:

1. Hemoglobin ………………………………..
2. P. V. bleeding ……………………………..
3. Sight ………………………………………
4. Blood pressure ……………………………
5. Urine for routine examination ……………..
6. Stool for routine examination ………………..
7. Asthma ……………………………………….
8. Skin diseases ………………………………..
9. Leprosy ……………………………………..
10. Any deforminity ……………………………
11. Epilepsy ……………………………………..
12. Pulmonary tuberculosis …………………….
13. Neurosis …………………………………..
14. Venereal diseases ……………………….
15. Other serious diseases ……………………

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by Government Medical Officer

1. I have examined the above named pupil and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time schooling.
2. Other comments ………………………………………………………………..

Thank you,

Date: ………………………………………
Name ………………………………… and signature …………………….
Designation …………………………….
Official stamp